



# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



## TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

### TAARIFA KWA UMMA

#### KUHUSU RATIBA YA UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE KATIKA MAJIMBO MATATU NA UDIWANI KATIKA KATA SITA - TANZANIA BARA

Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilipokea barua kutoka kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye kwa kuzingatia kifungu cha 37(3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, aliitaarifu Tume uwepo wa nafasi wazi za Majimbo ya Uchaguzi ya Singida Kaskazini, Mkoa wa Singida, kuanzia tarehe 30 Oktoba, 2017, kufuatia aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo Ndugu Lazaro Nyalandu, kuvuliwa uanachama na Chama Cha Mapinduzi. Hivyo, kwa mujibu wa Ibara ya 71(1)(f) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, amepoteza sifa ya kuwa Mbunge. Na kwa upande wa Jimbo la Uchaguzi la Songea Mjini Mkoani Ruvuma, nalo liko wazi kuanzia tarehe 24 Novemba, 2017 kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo Ndugu Leonidas Tutubert Gama.

Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 113(1)(2) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, Tume imepokea Hati kutoka Mahakama Kuu Kanda ya Arusha, ikithibitisha kuwa Jimbo la Longido, Mkoa wa Arusha lipo wazi kuanzia tarehe 30 Oktoba, 2017 kufuatia Mahakama Kuu kufuta matokeo ya uchaguzi wa jimbo hilo na hivyo Ndugu Onesmo Ole Nangole aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo kupoteza sifa za kuwa Mbunge.

Wakati huo huo, Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, ameitaarifu Tume uwepo wa nafasi wazi za Madiwani katika Kata sita (6) Tanzania Bara.

Baada ya kupokea taarifa hizo na kwa mujibu wa vifungu vya 37 (1) (b) na 46 (2) vya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, ikisomwa pamoja na kifungu cha 13(3) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatoa taarifa kwa Umma kuwa majimbo matatu ya **Longido, Songea Mjini na**

**Singida Kaskazini yapo wazi na Kata za Kimandolu, Kihesa, Bukumbi, Kurui, Keza na Kwagunda zipo wazi.**

Majimbo na Kata hizo zimeoneshwa kwenye jedwali Na. 1 na Na. 2.

**Jedwali Na. 1: Majimbo ya Uchaguzi yaliyowazi**

Na.	Mkoa	Halmashauri	Jimbo lililowazi
1.	Arusha	Halmashauri ya Wilaya ya Longido	Longido
2.	Ruvuma	Halmashauri ya Manispaa ya Songea	Songea Mjini
3.	Singida	Halmashauri ya Wilaya ya Singida	Singida Kaskazini

**Jedwali Na. 2: Kata zilizowazi**

Na.	Mkoa	Halmashauri	Kata zilizowazi
1.	Arusha	Halmashauri ya Jiji la Arusha	Kimandolu
2.	Iringa	Halmashauri ya Manispaa ya Iringa	Kihesa
3.	Tabora	Halmashauri ya Wilaya ya Uyui	Bukumbi
4.	Pwani	Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe	Kurui
5.	Kagera	Halmashauri ya Wilaya ya Ngara	Keza
6.	Tanga	Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe	Kwagunda

Aidha, kwa kuzingatia masharti ya vifungu vya 37(1)(b) (5) na 46 (2) vya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, pamoja na vifungu vya 13(3) na 41(3) vya Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume inatoa taarifa wa Umma kuhusu Ratiba ya uchaguzi mdogo katika majimbo matatu na Kata Sita; kama ifuatavyo:

- 1. Kutoa Fomu za Uteuzi** katika Majimbo ya Singida Kaskazini na Longido na Kata za Keza, Kimandolu, Kwagunda, Bukumbi, Kurui na Kihesa itakuwa kati ya tarehe 12 hadi 18 Desemba, 2017.
- 2. Kutoa Fomu za Uteuzi** katika Jimbo la Songea Mjini itakuwa kati ya tarehe 14 hadi 20 Desemba, 2017.
- 3. Uteuzi wa Wagombea** katika Majimbo ya Singida Kaskazini na Longido na Kata za Keza, Kimandolu, Kwagunda, Bukumbi, Kurui na Kihesa utafanyika **tarehe 18 Desemba, 2017**

4. **Uteuzi wa Wagombea** katika Jimbo la Songea Mjini utafanyika **tarehe 20 Desemba, 2017**
5. **Kampeni za Uchaguzi mdogo** katika Majimbo ya Singida Kaskazini na Longido na Kata za Keza, Kimandolu, Kwagunda, Bukumbi, Kurui na Kihesa zitaanza tarehe **19 Desemba, 2017 na kumalizika tarehe 12 Januari, 2018.**
6. **Kampeni za Uchaguzi mdogo** katika Jimbo la Songea Mjini zitaanza tarehe **21 Desemba, 2017 na kumalizika tarehe 12 Januari, 2018.**
7. **Siku ya uchaguzi** katika Majimbo ya Singida Kaskazini, Longido na Songea Mjini na Kata za Keza, Kimandolu, Kwagunda, Bukumbi, Kurui na Kihesa itakuwa **tarehe 13 Januari, 2017.**

Tunavikumbusha Vyama vya Siasa na wadau wote wa uchaguzi wazingatie Sheria, Kanuni, Taratibu, Miongozo na Maelekezo yote wakati wa kipindi cha uchaguzi mdogo wa majimbo matatu na Kata Sita.

Imetolewa leo tarehe 02 Desemba, 2017 na;

Mhe. Jaji Mkuu (Mst. Zanzibar) Hamid Mahmoud Hamid  
**MAKAMU MWENYEKITI**  
**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**